# MATIBABU YA JAMII YA KUSIMAMIWA KWA WAGONJWA WA SEHEMU YA 3

( Sehemu ya 17A ya Sheria ya Afya ya Akili 1983)

| | |
|---|---|
| 1. Jina la Mgonjwa | |
| 2. Jina la mtu anayekutunza (“daktari wako anayewajibika”) | |
| 3. Tarehe ambayo matibabu ya jamii ya kusimamiwa yataanza | |

## Je! ni kwanini niko kwenye matibabu ya jamii ya kusimamiwa?

Uko kwenye matibabu ya jamii yakusimamiwa chini ya sehemu ya 17A ya Sheria ya Akili 1983 kwa sababu mtu anayesimamia utunzaji wako (daktari wako anayewajibika) anafikiria umepona vizuri kiasi cha kutoka hospitalini lakini ana wasiwasi kuwa unaweza kukosa kuendelea na matibabu yako, au unaweza hitajika kulazwa hospitalini tena kwa ilani fupu kwa matibabu zaidi.

Matibabu ya jamii ya kusimamiwa inamaanisha kuwa timu yako ya utunzaji itafanya vyema iwezavyo kukusaidia kukaa vizuri baada ya wewe kuruhusiwa kutoka hospitalini, lakini ikiwa daktari wako anayewajibika anafikiria unahitaji matibabu tena, unaweza kuambiwa urudi hospitalini kwa matibabu uanayohitaji.

Daktari wako anayewajibika atazungumza nawe kuhusu mipango ya matibabu na utunzaji unaohitaji kwa shida yako ya akili kufuatia kuruhusiwa kwako kutoka hospitalini.

## Je! amri ya matibabu ya jamii ni nini?

Amri ya matibabu ya jamii ni fomu ambayo daktari wako anayewajibika na mtaalam wa afya ya akili aliyeidhinishwa lazima wajaze kusema kuwa unapaswa kuwa kwenye matibabu ya jamii ya kusimamiwa.

Mtaalam wa afya ya akili aliyeidhinishwa ni mtu ambaye amefunzwa kwa njia maalum kusaidia kuamua ikiwa watu wanahitaji kuwekwa hospitalini chini ya Sheria ya Afya ya Akili.

## Je! ni nini hufanyika nikitoka hospitalini?

Daktari wako anayewajibika atazungumza nawe kuhusu nini hufanyika kwenye matibabu ya jamii ya kusimamiwa.

Labda utaulizwa kufanya mipango fulani ya matibabu yako. Au mipango nyingine kukusaidia kuishi salama na vizuri katika jamii. Haya yanaitwa "masharti", na yanakubalika chini ya sehemu ya 17B ya Sheria ya Afya ya Akili.

Daktari wako anayewajibika na mtaalam wa afya ya akili aliyeidhinishwa lazima wakubaliane kuwa masharti haya yanafaa, na watapanga msaada wowote unaoweza kuhitaji kuyahifadhi. Unapaswa kuzungumza na daktari wako ikiwa una wasiwasi kwa sababu yoyote kuhusu jambo lolote utakaloulizwa kufanya, au kutofanya, wakati uko kwenye matibabu ya jamii ya kusimamiwa.

## Je! ni nini kitakachofanyika ikiwa sitafuata masharti?

Ikiwa hautafuata masharti timu yako ya utunzaji itahitaji kufikiria kama unahitaji kurudi hospitalini kwa matibabu.

Unaweza kaumbiwa urudi hospitalini ikiwa daktari wako anayewajibika anafikiria hii ndio njia pekee ya kuhakikisha kuwa unapata matibabu unayohitaji. Wakati mwingine hii inaweza hitajika ikiwa umefauta masharti yote. Hii inaitwa "kuitwa tena" hospitalini.

Ikiwa daktari wako anayewajibika anafikiria unahitaji kuitwa tena hospitalini, daktari wako atakumbia kwa kuandika kuwa unahitaji kuja hospitalini mara moja, au kwa wakati fulani. Ikiwa hautakuja unapoambiwa, unaweza kuletwa hospitalini kinyume na mapenzi yako.

Ikiwa utaitwa tena hospitalini, unaweza kuwekwa huko kwa muda wa hadi masaa 72. Ikiwa daktari wako anayewajibika anafikiria unahitaji kukaa hospitalini kwa muda mrefu zaidi, mtaalam wa afya aliyeidhinishwa ataulizwa azungumze nawe. Hii itafafanuliwa kwako wakati huo.

## Je! ni matibabu gani ninapaswa kupata wakati niko kwenye matibabu ya jamii ya kusimamiwa?

Daktari wako anayewajibika atajadiliana nawe kuhusu mahitaji yako ya matibabu na yatafanya kazi tu wakati na vile utatibiwa katika jamii.

## Je! ninaweza kukataa kutibiwa?

Una haki ya kukataa matibabu ikiwa hautaki, lakini hii inaweza maanisha kuwa daktari wako atahitajika kufikiria kukuita tena hospitalini.

Ikiwa hautaki matibabu hayo basi inaonyesha kuwa, unapaswa kuzungumza na daktari wako anayewajibika haraka iwezekanavyo.

## Je! na nikiwa mgonjwa sana kuamua kama nitakubali matibabu yangu?

Ikiwa watu wanaokutibu wanafikiria hauna uwezo wa kuamua wewe mwenyewe kama utatibiwa, wanaweza kukupa matibabu ikiwa wanafikiria unahitaji.

Lakini hawawezi kukulazimisha kukubali matibabu ikiwa unapinga, isipokuwa kama ni hali ya dharura.

“Ukosefu wa uwezo” unamaanisha kuwa, kwa sababu ya shida yako ya akili, hauwezi kufanya moja au zaidi ya mambo yafuatayo:

- Kuelewa habari uliyopewa juu ya matibabu
- Kuweka habari hiyo kwa muda mrefu ili kuweza kufanya uamuzi
- Kupima habari uliyopewa ili kufanya uamuzi
- Kuelezea uamuzi wako kwa njia yoyote ile, kama kuzungumza, kutumia lugha ya ishara, au mienendo rahisi kama kupepesa macho au kufinya mkono

Isipokuwa ni hali ya dharura, hauwezi kupewa matibabu ikiwa umefanya uamuzi wa mapema unaofungwa kisheria kukataa chini ya Sheria ya Uwezo wa Kiakili 2005, au mtu mwingine anyaeruhusiwa kufanya uamuzi kwa niaba yako chini ya Sheria hiyo amesema kuwa haupaswi kupata matibabu hayo. Huyu anaweza kuwa mtu ambaye umempa uwezo wa wakili wa kudumu, makamu aliyeteuliwa kwako na Korti ya Ulinzi, au Korti ya Ulinzi yenyewe. Hospitali inaweza kukupa habari zaidi kuhusu Sheria ya Uwezo wa Akili 2005.

## Sheria maalum kuhusu matibabu ya dawa na madawa

Mara tu unapokuwa katika matibabu ya jamii ya kusimamiwa kwa mwezi moja, sheria fulani maalum kuhusa dawa na madawa zinatumika.

Ikiwa unapewa matibabu ya dawa au madawa kwa shida yako ya akili, na ni zaidi ya miezi tatu tangu wakati ulipewa matibabu kama haya kwa mara ya kwanza wakati ulipokuwa hospitalini au kwenye matibabu ya jamii ya kusimamiwa, utaulizwa kuruhusu daktari wa kujitegemea (ambaye hatoki kwenye hospitali ianayokutibu) akuchunguze.

Daktari huyu wa kujitegemea anaitwa SOAD (Daktari wa Maoni ya pili aliyewekwa) (Second Opinion Appointed Doctor) ni ameteuliwa naTume inayojitegemea ambayo inaangalia jinsi Sheria ya Afya ya Akili inatumika.

Daktari huyu ataangalia kama matibabu ni sawa kwako, na atazungumza nawe kabla ya kuamua ni matibabu gani utaendelea kupata.

Unaweza tu kupewa matibabu ya dawa au madawa ambayo huyu daktari wa kujitegemea amesema ni sawa kwako, isipokuwa  kama ni hali ya dharura.

Utaambiwa ni lini na wapi daktari wa kujitegemea anataka kukuchunguza. Kuona daktari wa kujitegemea ni moja ya masharti ya matibabu ya jamii ya kusimamiwa. Ikwa hautaona daktari wa kujitegemea wakati na mahali unapoambiwa, daktari wako anayewajibika anaweza kulazimika kukuita tena hospitalini kumuona daktari wa kujitegemea.

Kuna sheria tofauti za matibabu fulani maalum, kama Tiba ya Kuikisa kupitia stima (ETC). Ikiwa watu wanaokutibu wanafikiria unahitaji moja ya matibabu haya maalum, sheria zitafafanuliwa kwako.

## Je! ninapaswa kukaa kwa matibabu ya jamii ya kusimamiwa kwa muda gani?

Amri yako ya matibabu ya jamii ya kusimamiwa itakaa hadi miezi sita, isipokuwa daktari wako anayewajibika aamue haitajiki tena.

Utaulizwa kuruhusu daktari wako anayewajibika kukuchunguza mwisho wa miezi sita, kuona ikiwa unahitaji kukaa kwa matibabu ya jamii ya kusimamiwa. Utaambiwa ni lini na wapi daktari wa kujitegemea anataka kukuchunguza.

Komuona daktari wako anayewajibika kwa uchunguzi ni moja ya masharti ya matibabu ya jamii ya kusimamiwa. Ikiwa hautamuona daktari wako kwa wakati au mahali ulipoambiwa, daktari wako anayewajibika anaweza kukuita tena hospitalini ili akuchunguze.

Ikiwa daktari wako anayewajibika anafikiria unahitaji kukaa kwa matibabu ya jamii ya kusimamiwa kwa muda zaidi, anaweza kuongeza muda hadi miezi sita zaidi, alafu hadi mwaka moja. Daktari wako anayewajibika atazungumza nawe kuhusu haya ukielekea mwisho wa kipindi hicho.

## Je! ninaweza kuomba rufaa?

Ndio. Unaweza kuuliza wasimamizi wa Hospitali yako ianayowajibika kusitisha matibabu ya jamii ya kusimamiwa. Unaweza kufanya hivi wakati wowote. Wasimamizi wa Hospitali ni kamati maalum ya watu waliowekwa katika hospitali kuamua kama watu bado wanahitaji matibabu ya jamii ya kusimamiwa.

Hospitali yako ianayowajibika kawaida ni hospitali uliyokuwa kabla ya kuenda kwenye matibabu ya jamii ya kusimamiwa. Ikiwa daktari wako anayewajibika atabadilika utaambiwa.

Ikwa unataka Wasimamizi wa Hospitali wasitishe matibabu ya jamii ya kusimamiwa, unaweza kuwaandikia kwa:

| |
|---|
| |

Wasimamizi wa Hospitali wanawezataka kukuzungumzia kabla ya kuamua kama kusitisha matibabu ya jamii ya kusimamiwa.

Jamaa wako wa karibu zaidi anaweza kuambia Wasimamizi wa Hospitali kuwa anataka matibabu ya jamii ya kusimamiwa yaishe. Kijikaratasi hiki kinafafanua zaidi jamaa wako wa karibu zaidi ni nani.

Ikiwa jamaa wako wa karibu atafanya hivi, matibabu yako ya jamii ya kusimamiwa yataisha baada ya masaa 72, isipokuwa daktari wako anayewajibika aambie Wasimamizi wa Hospitali kuwa unaweza kuwa hatari kwako na watu wengine ikiwa utaacha kuwa kwenye matibabuya jamii ya kusimamiwa. Ikiwa hii itafanyika, itakuwa miezi mingine sita kalba ya jamaa wako wa karibu waweze kuambia Wasimamizi wa Hospitali kuwa wanataka kusitisha matibabu ya jamii ya kusimamiwa.

Unaweza pia uliza Mahakama kusema kuwa matibabu ya jamii ya kusimamiwa yanapaswa kuisha.

## Mahakama ni nini na nini hufanyika?

Mahakama ni jopo la kujitegemea ambalo linaweza kuamua kama matibabu yako ya jamii ya kusimamiwa yanapaswa kuisha. Itafanya mkutano na wewe na wafanyikazi wanaokujua kutoka kwa hospitali hiyo. Mkutano huu unaitwa “usikilizaji”. Unaweza kumuuliza mtu mwingine aje kwenye usikilizaji huo kukusaidia. Kabla ya usikilizaji, washiriki wa Mahakama watasoma ripoti kukuhusu na utunzaji wako kutoka kwa hospitali. Mmoja wa washiriki wa mahakama pia watakuja kuzungumza nawe.

## Je! ni lini ninaweza kutuma ombi kwa mahakama?

Unaweza kutuma ombi kwenye Mahakama mara moja wakati wowote katika miezi sita ya kwanza ya ulezi wako. Unaweza pia kutuma ombi mara moja katika miezi sita inayofuata na kisha kila mwaka ambao unakaa katika matibabu ya jamii ya kusimamiwa baada ya hayo.

Ikiwa jamaa wako wa karibu zaidi aliambia hospitali kuwa wanataka matibabu yako ya jamii ya kusimamiwa yasitishwe, lakini daktari wako anayewajibika alisema kuwa hayapaswi kuisha, jamaa wako wa karibu zaidi anaweza kutuma ombi kwa Mahakama. Jamaa wako wa karibu zaidi lazima afanye hivi katika siku 28 za kaumbiwa kuwa daktari wako anayewajibika hakufikiria kuwa unapaswa kuruhusiwa kutoka hospitalini.

Ikiwa unataka kuomba kwa Mahakama unaweza kuandika kwa:

The Tribunals Service
PO BOX 8793
5th Floor
Leicester
LE1 8BN Simu 0300 123 2201

Unaweza kumuuliza wakili aandikie Mahakama kwa usaidizi wako katika usikilizaji. Hospitali yako inayowajibika na Shirika la Sheria wana orodha ya wakili ambao wana utaalam katika haya. Hautahitajika kulipa kwa usaidizi wa wakili kwa haya. Ni bure chini ya Mpango wa Usaidizi wa Kisheria.

## Kumjulisha jamaa wako wa karibu zaidi

Nakala ya kijikaratasi hiki kitapewa mtu ambaye Sheria ya Afya ya Akili inasema ni jamaa wako wa karibu zaidi.

Kuna orodha ya watu katika Sheria ya Afya ya Akili ambao wanachukuliwa kama jama. Kwa kawaida, mtu anayekuja juu kabisa kwenye orodha ndiye jamaa wako wa karibu zaidi. Wafanyikazi wa hospitali wanaweza kukupa kijikaratasi kinachoeleza haya na ni haki gani  jamaa wako wa karibu zaidi anazo kuhusiana na utunzaji na matibabu yako.

Katika hali yako, tumeambiwa kuwa jamaa wako wa karibu zaidi ni:

| |
|---|
| |

Ikiwa hautaki huyu mtu apokee nakala ya kijikaratasi hiki, tafadhali mjulishe mlezi wako, mfanyikazi wa jamii au mtu aliyekupa kijikaratasi hiki.

## Kubadilisha jamaa wako wa karibu zaidi

Ikiwa haufikirii kuwa mtu huyu anafaa kuwa jamaa wako wa karibu zaidi, unawezaomba mtu mwingine achukuliwe kama jamaa wako wa karibu zaidi badala yeke kwenye Korti ya Mkoa. Wafanyikazi wa hospitali wanawezakupa kijikaratasi kinachofafanua haya.

## Kanuni za Kufanya kazi

Hii ni Kanuni ya Kufanya kazi ambayo inakupa ushauri kuhusu Sheria ya Afya ya Akili kwa watu wanaohusika katika utunzaji wako. Wafanyikazi wanapaswa kuzingatia Kanuni inasema nini wakati wanapofanya uamuzi kuhusu utunzaji wako. Unaweza kuuliza nakala ya Kanuni, ikiwa unataka.

## Ninapaswa kulalamika aje?

Ikiwa unataka kulalamika kuhusu jambo lolote linalohusiana na utunzaji wako na matibabu katika hospitali tafadhali ongea na mfanyikazi. Hii inaweza kusaidia kutatua swala hilo. Wanaweza kupa habari kuhusu utaratibu wa malalamishi ya hospitali, ambayo unaweza kutumia kujaribu kutatua malalamishi yako kupitia jambo linaitwa suluhisho za kawaida. Wanaweza pia kukuambia kuhusu watu wengine wowote ambao wanaweza kukusadia kulalamika.

Unaweza kulalamika kwa Tume ya kujitegemea. Tume hiyo huchunguza jinsi Sheria ya Afya ya Akili inatumika, kuhakikisha inatumiwa vyema na kuwa wagonjwa wanatunzwa vyema wakiwa hospitalini. Wafanyikazi wa hospitali wanaweza kukupa kijikaratasi kinachofafanua jinsi ya kuwasiliana na Tume.

## Usaidizi na habari zaidi

Ikiwa kuna jambo lolote ambalo hauelewi kuhusu utunzaji wako na matibabu yako, wafanyikazi watajaribu kukusaidia. Tafadhali uliza mfanyikazi kukufafanulia ikiwa kuna jambo lolote katika kijikaratasi hiki ambalo hauelewi au ikiwa una maswali mengine ambayo kijikaratasi hiki hakijajibu.

Tafadhali uliza nakala nyingine ya kijikaratasi hiki ukitaka kumpa mtu mwingine.